



THE KENYA NATIONAL EXAMINATIONS COUNCIL

**SCHOOL BASED ASSESSMENT
KISWAHILI SEHEMU A**

Gredi ya 8

SEPTEMBER/OKTOBER 2026

NAKALA YA MWALIMU

Sehemu A inatathmini Stadi ya Kusikiliza na Kuzungumza. Inajumuisha mazoezi matatu:

- i. Mazungumzo ya ana kwa ana
- ii. Ufahamu wa Kusikiliza
- iii. Kusoma kwa sauti

MUDA: Dakika 15 kwa kila mwanafunzi.

Maagizo ya jumla

1. Mwalimu awafahamishe **wanafunzi wote** kwamba mazoezi yote katika sehemu hii yatakuwa ya ana kwa ana. Kila mwanafunzi atakuwa na zamu yake ya kutathminiwa; mmoja baada ya mwingine.
2. Mwalimu awafahamishe wanafunzi wote kwamba karatasi hii ina mazoezi matatu:
 - i. **Mazungumzo ya ana kwa ana**
 - ii. **Ufahamu wa Kusikiliza**
 - iii. **Kusoma kwa Sauti**
3. Mwanafunzi aandaliwe kiti au dawati kutazamana na mwalimu.
4. Mwalimu atangulize kila zoezi na amfahamishe mwanafunzi matarajio ya kila zoezi.
5. Mwalimu amfahamishe mwanafunzi kukamilika kwa kila zoezi.
6. Mwalimu atathmini umilisi wa mwanafunzi kwa mujibu wa mwongozo wa kutathminia pamoja na kuweka rekodi.

ZOEZI IA: MAZUNGUMZO YA ANA KWA ANA

Maagizo maalum

- i. *Andaa mazingira mazuri ya tathmini kwa kumkaribisha mwanafunzi.*
- ii. *Mwamkue na kumwomba akae.*
- iii. *Jitambulisha kwake kwa kusema, 'Mimi ni mwalimu_____'.*
- iv. *Muulize jina lake.*
- v. *Anza tathmini kwa kusema,*

“Wanyama ni viumbe wanaostahili kutunzwa vyema. Hata hivyo, wao hukumbwa na changamoto mbalimbali. Leo tutazungumza kuhusu changamoto zinazowakumba wanyama.”

1. Hebu nitajie mojawapo ya changamoto zinazowakumba wanyama.
(Mwanafunzi ajibu)
2. Wakazi wa kijiji chenu hawajali maslahi ya wanyama. Je, utawapa ushauri gani kuhusu umuhimu wa kuwatunza?
(Mwanafunzi ajibu)
3. Jirani yenu ana mazoea ya kuwatesa wanyama. Utachukua hatua gani?
(Mwanafunzi ajibu)
4. Neno lingine lenye maana sawa na **changamoto** ni gani?
(Mwanafunzi ajibu)

ZOEZI IB: UFAHAMU WA KUSIKILIZA

Maagizo maalum

- i. Msomee mwanafunzi kifungu kifuatacho **mara mbili**.*
- ii. Mjulishe kuwa atajibu maswali baada ya kusomewa kifungu mara ya pili.*

Taifa letu lina jamii nyingi, nazo hupatikana katika maeneo tofautitofauti. Jamii hizi huishi kwa kuzingatia tamaduni ambazo hupitishwa kutoka kwa kizazi kimoja hadi kingine. Tamaduni hizi ndizo huitambulisha jamii na kuitofautisha na nyingine.

Ni muhimu kutambua kuwa kila jamii hujivunia utamaduni wake. Si ajabu kuipata jamii moja ikijivunia aina fulani ya chakula cha kiasili. Nyingine nazo huenda zikaonyesha baadhi ya mitindo ya kujirembesha, ya mavazi na hata ya kupiga ngoma. Kuna tamaduni zinazohusu shughuli za kijamii kama vile posa, arusi na hata matanga. Hizi zote hutarajiwa kufuatwa na kila mwanajamii. Huenda hata ukiwa mgeni ukahitajika kuzifuata tamaduni hizo.

Ikumbukwe kwamba utamaduni ni dira inayoongoza mahusiano ya kijamii. Hivyo, inatupasa kuzifuata tamaduni zetu na wakati huo huo kuziheshimu tamaduni za wengine. Aidha, pana haja ya kuepuka mazoea ambayo yanaweza kuhatarisha maisha yetu na ya wanajamii wengine.

5. Ni nini ambacho huitambulisha jamii?
(Mwanafunzi ajibu)
6. Kulingana na kifungu, unahitaji kufanya nini ili kuendeleza utamaduni wa jamii yako?
(Mwanafunzi ajibu)
7. Usipoheshimu tamaduni za wengine, unadhani kutatokea nini??
(Mwanafunzi ajibu)
8. Neno **hujivunia** limetumika kwenye kifungu kumaanisha nini?
(Mwanafunzi ajibu)

ZOEZI 2 : KUSOMA KWA SAUTI

Maagizo maalum

- i. *Mfahamishe mwanafunzi matarajio ya Zoezi la Kusoma. (Zingatia mwongozo wa kutathminia Kusoma kwa sauti).*
- ii. *Mpe mwanafunzi nakala atakayoisoma kwa sauti.*
- iii. *Mwanafunzi anaposoma, sikiliza na kurekodi idadi ya maneno anayosoma kwa muda wa **dakika moja**.*
- iv. *Onyesha kwa mshazari (/) mahali mwanafunzi alipofikia kusoma **dakika moja** ikikamilika.*
- v. *Mruhusu mwanafunzi kusoma mpaka mwisho wa kifungu.*
- vi. *Pigia mstari maneno **yote** ambayo mwanafunzi atashindwa kuyasoma au kuyatamka vizuri.*
- vii. *Rekodi idadi ya maneno ambayo mwanafunzi ameweza **kusoma kwa usahihi** kwa dakika **moja**. (Baada ya kuondoa yaliyotamkwa vibaya au/na aliyoshindwa kutamka)*
- viii. *Rekodi viwango vya umilisi wa mwanafunzi kwa kuzingatia mwongozo uliopewa.*
- ix. *Hakikisha una nakala ya kurekodia tathmini hii. (Iwe na majina ya wanafunzi wote.)*
- x. *Ukiwa tayari kuanza tathmini, sema,*
“Sasa naomba unisomee kifungu hiki kwa sauti.”

Mwalimu amwambie mwanafunzi asome kifungu kifuatacho kwa sauti.

Katika shughuli zetu za ujifunzaji, tunakutana na watu wengi, si¹⁰ shuleni tu bali pia katika mazingira ya nyumbani. Tunahimizwa kushirikiana²⁰ na wengine ili tuweze kujielimisha kwa njia ifaayo. Katika kushirikiana³⁰ huku, zipo nyakati ambapo tunajipata katika migogoro ambayo inaathiri mshikamano⁴⁰ wa kijamii. Je, tunawezaje kukabiliana na migogoro hii?

Ni vyema⁵⁰ kubuni mikakati ifaayo ili kusuluhisha migogoro baina yetu. Moja kati⁶⁰ ya mikakati hii ni kudhibiti mielekeo na hisia zetu. Tunafaa⁷⁰ tujifahamu na kuwaelewa wenzetu ili tubaini sababu ya kufanya wayafanyayo⁸⁰. Tunapowakosea wenzetu, tunafaa kuomba msamaha. Iwapo ni vigumu kuomba msamaha,⁹⁰ tunaweza kumhusisha mtu mwingine kama vile mwalimu au mshaurinasaha. Zaidi¹⁰⁰ ya yote, tuwe na marafiki//¹⁰⁵ ambao tutaweza kuongea nao wakati¹¹⁰ tunahisi kwamba tumekosewa. Marafiki hawa wataweza kutupatanisha ili kurejesha uhusiano¹²⁰ mwema tuliokuwa nao hapo awali¹²⁵.

HUU NDIO UKURASA WA MWISHO ULIOPIGWA CHAPA.